# INTERNATIONAL TRANSPORT WORKERS' FEDERATION

Karatasi ya Usuli ya ITF

Dira ya Kimataifa ya Viwango Salama, Barabara Salama, na Usafiri wa Barabarani Endelevu

JUNI 2023

INTERNATIONAL TRANSPORT WORKERS' FEDERATION

# DIRA YA ULIMWENGU KWA VIWANGO SALAMA, BARABARA SALAMA, NA SAFARI ZA BARABARANI ENDELEVU

## Mgogoro kwenye barabara zetu

Wafanyakazi wa usafiri wa barabarani ulimwenguni kote wanakabiliwa na shinikizo kubwa la kazi kutokana na mazoea ya bei duni ya utoaji zabuni, upangaji ratiba usio na sababu, na viwango vya chini vya malipo. Shinikizo hizi hutoka kwa kampuni zilizo juu ya minyororo ya ugavi ya kimataifa (kampuni za wateja au 'waajiri wa kiuchumi') na mtindo wa biashara unaotegemea kuegemea kupita kiasi kwa uwekaji kandarasi ndogo na kiwango cha ushindani kupita kisha kuwa na uharibifu wa kihalisi. Matokeo yake ni kwamba madereva hulazimika kufanya kazi muda mrefu kupita kiasi, kuendesha gari wakiwa wamechoka, mwendo wa kasi, kupakia magari yao kupita kiasi, na kupuuza kukarabati magari zao ili tu kujikimu. Hali hii inafanya barabara kuwa hatari kwa kila mtu.

Kila mwaka, watu wapatao milioni 1.3 hupoteza maisha yao na hadi watu milioni 50 kujeruhiwa katika ajali barabarani. Licha ya kuwa magari ya kibiashara ni sehemu ndogo tu ya magari yote barabarani, magari haya yanahusika katika asilimia 10 hadi 22 ya ajali zote kwa jumla.[1] Takriban watu 600 hufa kila mwaka katika ajali za lori nchini Afrika Kusini,[2] karibu watu 1000 nchini Korea Kusini,[3] na zaidi ya watu 5000 nchini Marekani.[4]

Bila Viwango Salama na utekelezaji thabiti, wafanyakazi wahamiaji walio katika mazingira magumu wanaonyanyaswa kwa viwango vya chini vya mishahara mara nyingi hulengwa na mashambulizi makali ya chuki dhidi ya wageni kutoka kwa madereva wengine wanao ogopa kupoteza ajira zao na kuwa maskini. Wafanyakazi wanazozana wao kwa wao huku wale walio juu ambao kwa hakika ndio wasababishao mazingira hatarishi ya ushindani wakiepuka uwajibikaji.

Wakiwa wamebanwa kutoka juu na shinikizo kutoka kwa waajiri wa kiuchumi wa kimataifa na kutoka chini na makampuni ya chini ambayo yanapata faida zao kwa njia haramu na za unyonyaji, waendeshaji wa usafiri wanaoweza kuwajibika wanalazimishwa

---

[1] *Miongozo ya ILO. 2019 ya kukuza kazi zenye staha na usalama barabarani katika sekta ya usafiri, 1.*

[2] *Shirika la Usimamizi wa Usafiri Barabarani. "Ajali mbaya za Lori na Basi nchini Afrika Kusini," March 2023.*

[3] *Hifadhi ya takwimu ya KoRoad TAAS.*

[4] *Utawala wa Usalama wa Magari ya mizigo wa Shirikisho la Marekani*

kuingia katika ushindani mkali na kuishia kukwepa gharama za kijamii na kimazingira au kusukumwa nje ya sekta hiyo.

Kiasi kikubwa cha madereva, haswa wale walionunua magari yao na kuziwajibikia, wanakabiliwa na deni linalo ongeza mkazo mwingine kwa familia na maisha ya kibinafsi. Masharti haya madogo yamesababisha ongezeko kubwa la madereva na uhaba katika nchi nyingi, ingali malipo yanasalia kuwa chini. Masharti yasiyo endelevu yanamaanisha kuwa wafanyakazi haswa wanawake huwa na wakati mgumu kuingia na kubaki sokoni, wakati wafanyakazi vijana mara nyingi hujiepusha kabisa na taaluma ya udereva wa kibiashara.

# Uwepo wa sekta ya usafiri wa barabarani iliyo bora, salama na endelevu inawezekana

**Haifai kuwa hivi.**

Tunaweza kuwa na ulimwengu ambapo usafiri barabarani ni salama kwa kila mtu, bidhaa na vifaa muhimu vinasafirishwa na wafanyakazi walio na hali nzuri na salama na ambapo makampuni yanashirikiana na wafanyakazi ili kuboresha ubora wa huduma na kuafikia malengo ya kijamii na kimazingira.

Katika ulimwengu kama huo, madereva wanafurahia viwango bora, usawa, na salama bila kujali utaifa wao, jinsia yao na kwa hivyo hawakabiliwi na hatari ya ushindani. Wahusika wote wa mnyororo wa ugavi (ikiwa ni pamoja na makampuni ya usafiri, usambazaji na wateja) wanao wajibu wa kuzingatia na kutekeleza viwango, serikali huchukua jukumu kubwa katika kudhibiti usawa, na jukumu kuu la vyama vya wafanyakazi katika michakato hii linatambuliwa na kuungwa mkono.

Katika ulimwengu kama huo, wanawake na wafanyikazi wachanga wanavutiwa na tasnia kwa faida inayotoa ikiwa ni pamoja na mafunzo, malipo mazuri, na kujipa muda sawa wa maisha-kazi. Faida kama hizo huhakikisha uwepo wa kutosha wa madereva wenye ujuzi ambao wanaweza kushiriki mahitaji makubwa ya huduma za barabara.

Sekta ya usafiri wa barabarani yenye haki, salama na endelevu inawezekana. Hili linaweza kuafikiwa kupitia Viwango salama vya kimataifa.

# Kwa nini twahitaji kampeni ya kimataifa ya Viwango Salama

Kila mfanyakazi anastahili kurudi nyumbani salama mwishoni mwa siku yake ya kazi. Cha kusikitisha ni kwamba katika usafiri wa barabarani hatari ya kutofika nyumbani ni kubwa mno. Ajali za barabarani sasa ndio sababu ya nane ya chanzo cha vifo vyote ulimwenguni. Idadi kubwa ya ajali mbaya huhusisha magari ya kibiashara. Kwa wafanyakazi wa usafiri wa barabarani, ambao mahali pao pa kazi ni barabarani, hatari ni kubwa, sio tu kwa sababu mara nyingi wanatumia zaidi ya saa 60 au 70 kwa wiki barabarani, lakini kutokana na ukubwa na uzito wa magari ya biashara wanayoyoendesha. Ajali inayohusisha gari la mizigo kubwa ina uwezekano mkubwa wa

kusababisha majeraha mabaya, na hivyo kuwaweka hatarini sio tu wafanyikazi, bali pia watumiaji wote wa barabara.

Athari za kimwili na kiakili zinazowapata madereva kutokana na hali zao za kazi huchangia pakubwa hatari za kiafya na kiusalama. Utafiti umegundua kuwa masaa mengi ya kazi kwa madereva wa lori husababisha shinikizo la damu, ugonjwa wa moyo na mishipa, na hatari ya kiharusi.[5] Utafiti pia umeonyesha kwamba madereva kwa hiari yao hupunguza muda wao wa kufanya kazi iwapo malipo yao yatatosha kulisha familia zao na kulipa gharama zao na pia kama wanalipwa kwa muda wa kazi zinginezo kando na kuendesha gari (kama vile muda wa kupakia/kupakua, muda wanaoupotezea kwenye vivukio vya mipaka na muda wa kusubiri kwenye msongamano wa magari).[6]

Ushahidi kutoka Marekani, Australia na Korea umethibitisha kwamba malipo bora kwa madereva huchangia kupunguka kwa idadi ya ajali barabarani, kuboresha usalama barabarani, na ni muhimu katika kufanya sekta hiyo kuwa endelevu zaidi.[7] Tafiti mbalimbali zimegundua kuwa malipo ya juu kwa 1% yanaweza kupunguza ajali za madereva wa lori kutoka kati ya 1 hadi 3%.[8] Tafiti zingine zimeonyesha uhusiano kati ya minyororo mirefu ya ukandarasi na ajali za barabarani, na kuonyesha kuwa kutekeleza viwango vya malipo kwa kampuni zilizoko juu ya minyororo hii husaidia kupunguza ukandarasi mdogo.[9]

Ni bayana kwamba, viwango Salama vinaweza kuokoa maisha. Lakini hii haitawezekana kutokea kwa nia njema pekee.

## Viwango Salama ni vipi?

Kumlipa dereva ‘kiwango salama’ kunamaanisha kwamba analipwa haki yake kwa muda wote wa kazi na apate pesa za kutosha kumwezesha kuendesha gari kwa usalama na bado akamilishe kazi yake, awe na muda wa kutosha kuwa nyumbani, na kushughulikia familia yake. Ikiwa dereva anamiliki gari lake mwenyewe, kiwango salama lazima kihesabiwe ili kuhakikisha kwamba anaweza kulipia gharama za kulinunua, kukarabati, na kuliendesha. Hii inaitwa 'kurejesha gharama'.

---

[5] *Takahiko Kudo na Michael H. Belzer.2020. “Saa Nyingi za Kazi na Shinikizo la damu: Ushahidi kutoka kwa Data ya Utafiti wa NIOSH.” Sayansi ya Usalama, 129.*

[6] *Michael H. Belzer na Stanley A. Sedo. 2018. “Kwa Nini Madereva wa Malori ya Masafa Mrefu Hufanya Kazi Masaa Mengi Sana?”; Tathmini ya Kiuchumi na Mahusiano ya Kazi, 29(1), 59–79.*

[7] *Kwa orodha isiyo kamili ya utafiti huu tazama miongozo ya ILO kuhusu uendelezaji wa kazi zenye staha na usalama barabarani katika sekta ya usafiri.’, Annex I.*

[8] *Michael H. Belzer, Daniel A. Rodriquez na Stanley A. Sedo, 2002. “Kulipia Usalama: Uchambuzi wa Kiuchumi wa Athari za Fidia kwa Usalama wa Dereva wa Lori.” Utawala wa Usalama wa Magari ya mizigo wa Shirikisho la Marekani, Washington, D.C.; Daniel A. Rodríguez, na wengine., 2003. “Madhara ya Mishahara ya Dereva wa Lori na Masharti ya Kazi kwa Usalama Barabarani: Uchunguzi,” Rekodi ya Utafiti wa Usafiri, Sera ya Mizigo, Uchumi na Usafirishaji; Usafiri wa Lori (1833), 95-110’ Daniel A. Rodríguez, Felipe Targa, na Michael H. Belzer, 2006. “Motisha ya malipo na Usalama wa Dereva wa Lori: Uchunguzi kifani,” Tathmini ya Mahusiano ya Kazi Viwandani, 59(2), 205-225;*

[9] *KOTI, 2022. Mfumo wa Viwango Salama: Uchambuzi wa Utendaji na Hatua za Kuboresha. Iliyoagizwa na ROK Wizara ya Ardhi, Miundombinu na Uchukuzi Ministry of Land, Miundombinu na Usafiri [ya Korea]; Gwanghun Lee na Taesung Kim, 2017. Utafiti kuhusu Athari za Mazingira ya Kazi ya Usafirishaji wa Malori ya Korea kwenye Ajali za Barabarani [ya Korea].*

Wanabiashara wa usafiri pia wanapaswa kurejesha gharama zao huku wakizingatia haki na hali salama kwa madereva wao. Maanake, bei ya usafiri barabarani lazima iwe sawa, na iangazie gharama zote za kijamii.

‘Mfumo wa Viwango Salama’ hurejelea mfumo wa udhibiti wa kisheria ambao kima cha chini kabisa cha viwango vya malipo na yale masharti yanayohusiana na kufanya kazi vimewekwa kwa lengo la kutokomeza shinikizo kwa madereva kujihusisha na tabia hatari barabarani.

Cha muhimu ni kwamba, mifumo ya Viwango Salama inawalazimisha kisheria makampuni yaliyo juu ya minyororo ya ugavi wa usafiri barabarani ili kuhakikisha uzingatiaji wa viwango hivi.

Kanuni kuu za mifumo ya Viwango Salama ni:

01. Viwango nafuu na sawa kwa madereva **<u>wote</u>** bila kujali aina ya ajira (au tofauti zingine kama vile utaifa au jinsia).
02. Majadiliano ya kisheria na wadau wa kuweka viwango
03. Vyama vyote vilivyo kwenye minyororo ya ugavi, hasa makampuni yaliyo juu ya mnyororo, wanawajibishwa.
04. Ufuatiliaji na utekelezaji thabiti
05. Vyama vya wafanyakazi vinahusishwa katika mchakato wa kuweka, ufuatiliaji na utekelezaji viwango kutoka mwanzo hadi mwisho.

## Kuhamisha nguvu kutoka kwa mtaji hadi kwa wafanyikazi kupitia Viwango Salama

Iwe imepachikwa katika makubaliano na waendeshaji na wateja wa usafiri, au katika mifumo ya udhibiti wa kisheria, Viwango Salama vinaokoa maisha kwa kuboresha malipo na masharti na kupunguza shinikizo la kuendesha gari kwa njia hatari.

Hata muhimu zaidi, Viwango Salama ni msingi wa kujenga umoja na nguvu za wafanyakazi na kutumia uwezo huu kuunda upya sekta ya usafiri wa barabarani. Kupigania Viwango Salama huwaleta pamoja wafanyakazi kutoka kwa makampuni mbalimbali, kutoka aina kadha za ajira na mataifa tofauti ambao vinginevyo wanalazimishwa kuwa katika ushindani baina yao na kwa pamoja kupigania viwango sawa na sekta ya uhaki, salama na endelevu, wakipeana nguvu kutoka chini.

Mifumo na mikataba ya Viwango Salama hutoa muundo wa kujadiliana na makampuni yaliyoko juu ya minyororo ya ugavi na kupachika vyama vya wafanyakazi katika mchakato wa kuweka, kufuatilia, na kutekeleza viwango, kuweka mamlaka hiyo katika taasisi, na kuunda msingi wa upangaji mpana zaidi. Mafanikio ya mkakati huu tayari yanaweza kuonekana katika mataifa kama vile Korea Kusini, Australia, Brazili na Canada.

# Umoja katika mapambano yetu

**Tayari tunashinda pambano la Viwango Salama!**

Tangu jimbo la Australia la New South Wales lilipoanzisha mfumo wa Viwango Salama kama sehemu ya mfumo wake wa mahusiano ya viwanda mwaka wa 1979, wafanyakazi na vyama vya wafanyakazi duniani kote wamekuwa wakipigania na kushinda Viwango Salama. Viwango Salama au mifumo sawiya sasa inapatikana nchini Australia, Brazili, Canada na Marekani (hususan uchumi wa gig). Nchini Korea Kusini mfumo wa Viwango salama uliowekewa kikomo ulifanya kazi kwa mafanikio kati ya 2020-2022 na wafanyikazi sasa wanapigania kurudisha mfumo huo na kuufanya kuwa wa kudumu.

Katika ngazi ya kimataifa, vyama vya usafiri wa barabarani vilikusanyika chini ya ITF ili kujishindia kanuni za Viwango Salama katika Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi. Kanuni muhimu zinazotaka kuwepo kwa taratibu za hesabu za viwango endelevu vya mishahara na utekelezaji kwa wahusika wote wa ugavi sasa zimejumuishwa katika 'Muongozo wa ILO kuhusu uendelezaji wa kazi zenye staha na usalama barabarani katika sekta ya usafiri', ambayo yalijadiliwa na kukubaliwa na chama cha wafanyakazi, serikali na wawakilishi wa waajiri mwakani 2019.

Mwongozo wa ILO unavipa vyama vya usafiri wa barabarani katika sehemu zote za dunia kote mfumo wa kushawishi serikali na wahusika wa ugavi kufikia udhibiti na makubaliano ya Viwango Salama. Muongozo unaweza kutumika kama zana ya kuandaa na kuelimisha, na kwa kuwafahamisha wanachama juu ya haki zao.

# Tasnia Unaokuwa Kubwa na msaada wa umma

Makubaliano ya sekta na umma kuhusu umuhimu wa udhibiti wa Viwango Salama yanaongezeka katika mataifa kote ulimwenguni. Kwa mfano:

- Nchini New Zealand, utafiti ulioidhinishwa na serikali uliokamilishwa mwaka wa 2021 ulitambua uhusiano kati ya usalama na malipo na tatizo la shinikizo la ugavi kwa wafanyakazi wa usafiri wa barabarani.[10] Kamati ya utatu imeanzishwa ili kutekeleza mapendekezo ya ripoti hii, ikiwa ni pamoja na kufafanua viwango vya malipo ya haki, masaa salama, na kazi wastani na kuandaa kanuni zinazohitajika. Viwango Salama vinaungwa mkono na Transporting New Zealand, chama kikuu cha tasnia ya uchukuzi nchini.
- Nchini Korea Kusini, vyama vyote vitatu vikuu vya sekta ya safari za lori vimetia saini makubaliano na Kitengo cha Mshikamano cha Wafanyakazi wa Utumishi wa Umma na Usafiri wa Korea Kusini (KPTU-TruckSol) kikitoa wito kwa mfumo wa kudumu na kupanuliwa wa Viwango Salama. Kura ya maoni ya umma iliyofanywa mwishoni mwa 2022 iligundua kuwa 74% ya Wakorea wanaunga mkono kuendelea kwa Viwango Salama.[11]

[10] *WorkSafe New Zealand, 2021. "Kudhibiti Hatari Zinazohusiana na Gari kutoka kwa Shinikizo la Msururu wa Ugavi," https://www.worksafe.govt.nz/research/managing/.*
[11] *https://mobile.newsis.com/view.html?ar_id=NISX20221209_0002117586*

- Nchini Australia, mfumo wa Viwango Salama uliopo katika jimbo la New South Wales tangu 1979 unaungwa mkono sana na tasnia na wanasiasa katika pande zote za wigo wa kisiasa. Mnamo Agosti 2022, kampuni kubwa za wateja wa usafiri wa barabarani ikiwa ni pamoja na maduka makubwa ya Woolworths na Coles, makampuni ya jukwaa kama vile Uber na DoorDash, waendeshaji wakuu wa usafiri, vyama vya sekta ya uchukuzi na Chama cha Wafanyakazi wa Uchukuzi (TWU) walitia saini mwito wa kuchukua hatua kwa ajili ya marekebisho ya kisheria. kuanzisha bodi ya kitaifa ya udhibiti yenye uwezo wa kuweka na kutekeleza viwango salama na vya haki kwa wafanyakazi wa usafiri wa barabarani katika shughuli za kawaida za usafiri na uchumi wa gig.[12]

## Jiunge na kampeni ya kimataifa ya Viwango Salama

**"Mtindo shindani wa biashara katika sekta ya usafiri wa barabarani umevunjika na unasababisha maafa."**

Tatizo la kimataifa linahitaji suluhisho la kimataifa. Ni lazima tuendeleze mwendo ambao tayari umeafikiwa na kuendelea kuhamasisha umma kuhusu mgogoro ulioko katika usafiri wa barabarani. Ni lazima tuzungumze kwa sauti moja, kupanga washirika katika sekta, na kupigania na kuafikia Viwango Salama katika miktadha ya ndani, kitaifa, kikanda na kimataifa.

Ndiyo maana ITF inatoa wito kwa vyama vyote vya usafiri wa barabarani kujiunga na mapambano ya kimataifa ya Viwango Salama Okoa maisha.

Jiunge na Kampeni ya kimataifa ya Viwango Salama kwa kuunga mkono matakwa haya:

**Mifumo ya Viwango Salama**: Kuanzisha mifumo mpya na/au kuimarisha mifumo iliyopo ya kuweka viwango vya haki na salama vya malipo na masharti. Mifumo hii lazima ihusishe wahusika wote wa ugavi, ikijumuisha kampuni za wateja, na iwafikie wafanyakazi wote wa usafiri wa barabarani pasipo na kuzingatia aina ya ajira, utaifa na jinsia.

- **Bei nafuu ya uchukuzi:** Hakikisha kwamba wafanyakazi wote wa usafiri wa barabarani wanalipwa vyema kwa muda wote waliofanya kazi na waendeshaji wa usafiri na wafanyakazi wanaomiliki magari yao wanaweza kurejesha gharama zao bila kukiuka kanuni za usalama barabarani.
- **Uwazi ulioimarishwa:** Hakikisha kwamba wafanyakazi wote wa usafiri wa barabara wanapata nakala za kandarasi za ajira na/au huduma zinazoelezea malipo ya haki na salama na masharti ya kazi.
- **Uzingatiaji kikamilifu na utatuzi wa ukiukaji:** Hakikisha ufuatiliaji na utekelezaji wa kutosha wa viwango, ikiwa ni pamoja na vifungu vya adhabu, sharti kwa wahusika wote katika ugavi (makampuni ya wateja, waendeshaji

[12] https://www.twu.com.au/press/major-transport-roundtable-backs-reform-to-set-industry-standards/

wa usafiri, wafanyakazi katika aina zote za ajira, na kadhalika) Hakikisha kwamba wafanyakazi wote wa usafiri wa barabara wanapata taratibu madhubuti za utatuzi wa mizozo, ambazo zinajumuisha na kutumika kwa wahusika wote wa ugavi.

- **Haki za vyama vya wafanyakazi:** Kutambua jukumu muhimu linalotekelezwa na vyama vya wafanyakazi vya kidemokrasia katika kuendeleza usalama na uendelevu katika minyororo ya ugavi wa usafiri wa barabarani, kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wa usafiri wa barabarani wanapata uwakilishi kwa vyama vya wafanyakazi vya kidemokrasia na kuwezesha jukumu la vyama vya wafanyakazi katika elimu ya wafanyakazi; ufuatiliaji, na kuboresha afya na usalama.
- **Viwango vya kimataifa**: Tekeleza Miongozo ya ILO kuhusu ukuzaji wa ajira wastaha na usalama barabarani

**WWW.ITFGLOBAL.ORG**

. WE MOVE THE WORLD .